

REF: PPR/11 - 2/12

**TAARIFA KWA UMMA KUHUSU BEI KIKOMO ZA MAFUTA AINA YA PETROLI KUANZIA
JUMATATU, TAREHE 19 DISEMBA 2011**

Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) inatangaza bei kikomo za bidhaa ya mafuta ya petroli hapa nchini. Bei hizi zitaanza kutumika kuanzia **Jumatatu, Tarehe 19 Disemba 2011**. Pamoja na kutambua bei kikomo za bidhaa mbalimbali za petroli nchi nzima, ni muhimu kuzingatia yafuatayo.

- (a) Bei za jumla na rejareja kwa aina zote za mafuta zimebadilika ikilinganishwa na toleo lililopita la tarehe 5 Disemba 2011. Katika toleo hili, bei za rejareja kwa aina zote za mafuta zimeshuka kama ifuatavyo: Petroli imeshuka kwa TZS 108.00/lita sawa na asilimia 5.41; Dizeli imeshuka kwa TZS 99.00/lita, sawa na asilimia 4.80 na Mafuta ya taa imeshuka kwa TZS 91.00/lita, sawa na asilimia 4.41. Mabadiliko haya ya bei za mafuta hapa nchini yametokana na kushuka kwa bei katika soko la dunia na kuongezeka kwa thamani ya Shilingi ya Tanzania ikilinganishwa na dola ya Marekani, (sarafu ambayo hutumika katika manunuzi ya bidhaa za mafuta kwenye soko la dunia). Kwa kulinganisha toleo hili na toleo lililopita thamani ya shilingi ya Tanzania imeongezeka thamani kwa asilimia 4.00. Bei za jumla kwa kulinganisha matoleo haya mawili zimebadilika kama ifuatavyo: Petroli imeshuka kwa TZS 107.56/lita sawa na asilimia 5.60, Dizeli imeshuka kwa TZS 99.55/lita, sawa na asilimia 4.96 na bei ya Mafuta ya Taa imeshuka kwa TZS 90.41/lita, sawa na asilimia 4.56.
- (b) Kwa mujibu wa Sheria ya Mafuta ya mwaka 2008, bei za bidhaa za mafuta ya petroli zitaendelea kupangwa na soko. EWURA itaendelea kuhamasisha ushindani kwa kutoa taarifa za bei kikomo za bidhaa za mafuta. Taarifa hizi zina lengo la kuwasaidia wadau kufanya maamuzi stahiki kuhusu manunuzi ya bidhaa za mafuta.
- (c) **Kampuni za mafuta zipo huru kuuza bidhaa za mafuta ya petroli kwa bei ya ushindani ilimradi bei hizo ziko chini ya bei kikomo (price cap)** kama ilivyokokotolewa na *fomula* iliyopitishwa na EWURA na ambayo ilichapwa kwenye Gazeti la Serikali Na. 5 la tarehe 9 Januari 2009 na marekebisho yaliyofanywa kupitia Tangazo la Serikali Na. 216 la Tarehe 29 Julai 2011.
- (d) Vituo vyote vya mafuta vinatakiwa kuchapisha bei za bidhaa za mafuta katika mabango yanayoonekana bayana na yakionyesha bei ya mafuta, punguzo, vivutio vya biashara au promosheni zinazotolewa na kituo husika. Pale ambapo inawezekana kuchagua, wateja wanashauriwa kununua bidhaa za mafuta kutoka kwenye vituo vinavyouza mafuta kwa bei ndogo zaidi ili kushamirisha ushindani. **Ni kosa kuuza mafuta bila kuweka mabango ya bei inayoonekana vizuri kwa wateja na adhabu itatolewa kwa kituo husika.**
- (e) Wanunuzi wanashauriwa kuhakikisha kuwa wanapata stakabadhi ya malipo inayoonesha jina la kituo, tarehe, aina ya mafuta yaliyonunuliwa na bei kwa lita. Stakabadhi hiyo ya malipo itatumika kama

kidhibiti cha mnunuzi wa mafuta endapo kutajitokeza malalamiko ya ama kuuziwa mafuta kwa bei ya juu kuliko bei kikomo; ama endapo utakuwa umeuziwa mafuta yenye kiwango cha ubora kisichofaa.

A: BEI ZA REJAREJA

Mji	Bei Kikomo		
	Petroli (TZS/LT)	Dizeli (TZS/LT)	Mafuta ya Taa (TZS/LT)
Dar es Salaam	1,882	1,976	1,958
Arusha	1,966	2,060	2,042
Arumeru	1,966	2,060	2,042
Karatu	1,984	2,078	2,060
Monduli	1,971	2,065	2,047
Ngorongoro (Loliondo)	2,023	2,116	2,099
Kibaha	1,887	1,980	1,963
Bagamoyo	1,893	1,987	1,969
Kisarawe	1,889	1,983	1,965
Mkuranga	1,892	1,985	1,968
Rufiji	1,910	2,003	1,986
Dodoma	1,941	2,034	2,017
Konooa	1,974	2,067	2,049
Kongwa	1,938	2,031	2,014
Mpwapwa	1,942	2,035	2,018
Iringa	1,946	2,040	2,022
Kilolo	1,951	2,044	2,026
Ludewa	2,012	2,106	2,088
Makete	2,005	2,099	2,081
Mufindi	1,956	2,049	2,032
Njombe	1,974	2,068	2,050
Bukoba	2,097	2,191	2,173
Biharamulo	2,071	2,165	2,147
Chato	2,068	2,162	2,144
Karagwe	2,113	2,207	2,189
Muleba	2,097	2,191	2,173
Ngara	2,063	2,156	2,139
Misenyi	2,106	2,199	2,181
Kigoma	2,113	2,206	2,189
Kasulu	2,099	2,192	2,175
Kibondo	2,077	2,171	2,153
Moshi	1,956	2,049	2,032
Hai	1,959	2,052	2,035
Mwanga	1,949	2,042	2,025

Rombo	1,977	2,070	2,053
Same	1,942	2,036	2,018
Siha	1,962	2,056	2,038
Lindi	1,941	2,034	2,017
Kilwa Masoko	1,916	2,009	1,992
Liwale	1,962	2,055	2,038
Nachingwea	1,970	2,063	2,046
Ruangwa	1,968	2,062	2,044
Babati	2,004	2,098	2,080
Hanang	2,015	2,108	2,091
Kiteto	2,015	2,109	2,091
Mbulu	2,017	2,110	2,093
Simanjiro	2,036	2,130	2,112
Musoma	2,060	2,154	2,136
Bunda	2,051	2,145	2,127
Serengeti	2,106	2,199	2,182
Tarime	2,071	2,165	2,147
Mbeya	1,989	2,082	2,065
Chunya	1,999	2,092	2,074
Ileje	2,002	2,096	2,078
Kyela	2,005	2,098	2,081
Mbarali	1,973	2,067	2,049
Mbozi	1,998	2,092	2,074
Rungwe	1,998	2,091	2,074
Morogoro	1,907	2,001	1,983
Mikumi	1,923	2,016	1,999
Kilombero	1,945	2,038	2,021
Mahenge	1,956	2,049	2,031
Kilosa	1,926	2,019	2,001
Mvomero	1,918	2,011	1,994
Mtwara	1,954	2,048	2,030
Masasi	1,980	2,073	2,056
Newala	1,986	2,080	2,062
Tandahimba	1,980	2,073	2,055
Mwanza	2,032	2,125	2,108
Geita	2,073	2,166	2,149
Kwimba	2,068	2,161	2,144
Magu	2,040	2,133	2,116
Misungwi	2,038	2,131	2,113
Sengerema	2,064	2,158	2,140
Ukerewe	2,091	2,185	2,167
Sumbawanga	2,055	2,148	2,131
Mpanda	2,090	2,183	2,166
Nkasi	2,068	2,161	2,144
Songea	2,005	2,099	2,081

Mbinga	2,039	2,132	2,115
Namtumbo	2,035	2,128	2,111
Tunduru	2,064	2,158	2,140
Shinyanga	2,011	2,104	2,087
Kahama	2,024	2,118	2,100
Bukombe	2,037	2,130	2,113
Bariadi	2,052	2,145	2,128
Kishapu	2,039	2,132	2,115
Maswa	2,044	2,137	2,120
Meatu	2,051	2,144	2,127
Singida	1,973	2,066	2,049
Iramba	1,985	2,078	2,061
Manyoni	1,957	2,051	2,033
Tabora	2,036	2,129	2,112
Igunga	1,990	2,083	2,066
Nzega	2,001	2,094	2,077
Sikonge	2,048	2,141	2,124
Urambo	2,049	2,143	2,125
Tanga	1,928	2,022	2,004
Handeni	1,908	2,001	1,984
Kilindi	1,942	2,036	2,018
Korogwe	1,921	2,015	1,997
Lushoto	1,931	2,024	2,007
Mkinga	1,942	2,036	2,018
Muheza	1,928	2,022	2,004
Pangani	1,935	2,028	2,011

B: BEI ZA JUMLA

Bei za Jumla - DSM	Petroli	Dizeli	Mafuta ya Taa
Bei Kikomo	1,814.68	1,908.07	1,890.61

Haruna Masebu
MKURUGENZI MTENDAJI
EWURA